# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI YA 2016

---

## MPANGILIO WA VIFUNGU


**VIFUNGU** **MAELEZO**

**SEHEMU YA KWANZA**
**UTANGULIZI**

1. Jina fupi na kuanza kutumika.

**SEHEMU YA PILI**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAHUSIANO KAZINI, NAM. 1 YA 2005**

2. Kusomwa.
3. Marekebisho ya kifungu cha 81.

**SEHEMU YA TATU**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAHAKAMA ZA MAHAKIMU, NAM. 6 YA 1985**

4. Kusomwa.
5. Marekebisho ya kifungu cha 5.
6. Marekebisho ya kifungu cha 7.
7. Marekebisho ya kifungu cha 10.

**SEHEMU YA NNE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAHAKAMA YA BIASHARA ZANZIBAR, NAM. 9 YA 2013**

8. Kusomwa.
9. Marekebisho ya kifungu cha 37.

**SEHEMU YA TANO**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MADAWA NA USAMBAZAJI HARAMU WA MADAWA YA KULEVYA, NAM. 9 YA 2009**

10. Kusomwa.
11. Marekebisho ya kifungu cha 4.

12. Marekebisho ya kifungu cha 5.

13. Marekebisho ya kifungu cha 63.

**SEHEMU YA SITA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI, NAM. 8 YA 2015**

14. Kusomwa.

15. Marekebisho ya kifungu cha 2.

16. Marekebisho ya kifungu cha 21.

17. Marekebisho ya kifungu cha 35.

18. Marekebisho ya kifungu cha 38.

19. Marekebisho ya kifungu cha 46.

**SEHEMU YA SABA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA NAM. 4 YA 2015**

20. Kusomwa.

21. Marekebisho ya Jadweli la pili.

**SEHEMU YA NANE**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA BIASHARA NAM. 14 YA 2013**

22. Kusomwa.

23. Marekebisho ya kifungu cha 3.

24. Marekebisho ya kifungu cha 23.

**SEHEMU YA TISA**
**MAREKEBISHO YA SHERIA YA CHUO CHA KILIMO CHA KIZIMBANI, NAM. 5 YA 2007**

25. Kusomwa.

26. Marekebisho ya kifungu cha 7.

27. Marekebisho ya kifungu cha 9.

## SEHEMU YA KUMI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MFUKO WA JIMBO, NAM. 4 YA 2012


28. Kusomwa.

29. Marekebisho ya kifungu cha 9.


## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA ZANZIBAR, NAM. 7 YA 2014


30. Kusomwa.

31. Marekebisho ya kifungu cha 4.

32. Marekebisho ya kifungu cha 10.

33. Marekebisho ya kifungu cha 11.

34. Marekebisho ya kifungu cha 12.

35. Marekebisho ya kifungu cha 22.

36. Marekebisho ya kifungu cha 26.

37. Marekebisho ya kifungu cha 30.

38. Marekebisho ya kifungu cha 88.


## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI NAM. 4 YA MWAKA 1998


39. Kusomwa.

40. Marekebisho ya kifungu cha 3.

SHERIA NAMBA 5 YA 2016

NIMESAINI

{DR. ALI MOHAMED SHEIN}
RAIS WA ZANZIBAR NA MWENYEKITI
WA BARAZA LA MAPINDUZI

19th October, 2016

# SHERIA YA MAREKEBISHO YA SHERIA MBALIMBALI NA KUWEKA MASHARTI YALIYO BORA KUHUSIANA NA MAMBO HAYO

---

**IMETUNGWA** na Baraza la Wawakilishi la Zanzibar.

## SEHEMU YA KWANZA
## UTANGULIZI

Jina fupi na kuanza kutumika.

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali ya 2016 na itaanza kutumika mara baada ya kutiwa saini na Rais.

## SEHEMU YA PILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAHUSIANO KAZINI, NAM. 1 YA 2005

Kusomwa.

**2.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mahusiano Kazini, Nam. 1 ya 2005 ambayo katika Sehemu hii itajulikana kama Sheria mama.

Marekebisho ya kifungu cha 81.

**3.** Kifungu cha 81(1) cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta aya ya (a) na kuweka aya mpya ya (a) kama ifuatavyo:

"(a) Jaji wa Mahakama ya Kazi ya Zanzibar atateuliwa na Jaji Mkuu kutoka miongoni mwa Majaji wa Mahakama Kuu".

## SEHEMU YA TATU
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAHAKAMA ZA MAHAKIMU, NAM. 6 YA 1985

Kusomwa.

**4.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mahakama za Mahakimu, Nam. 6 ya 1985, na katika sehemu hii itajulikana kama Sheria mama.

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**5.** Kifungu cha 5(2) cha Sheria mama kinarekebishwa katika aya ya (a) kwa kufuta neno "cheti cha" liliopo baina ya neno "na" na "sheria" na kuweka badala yake maneno "Shahada ya Kwanza ya".

Marekebisho ya kifungu cha 7.

**6.** Kifungu cha 7 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kuingiza maneno "au Kiingereza" baada ya neno "Kiswahili".

Marekebisho ya kifungu cha 10.

**7.** Kifungu cha 10(2) cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "stashahada au" yaliyopo baina ya maneno "na" na "shahada".

## SEHEMU YA NNE
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAHAKAMA YA BIASHARA ZANZIBAR, NAM. 9 YA 2013

Kusomwa.

**8.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mahakama ya Biashara Zanzibar, Nam. 9 ya 2013, na katika sehemu hii itajulikana kama Sheria mama.

Marekebisho ya kifungu cha 37.

**9.** Kifungu cha 37 cha Sheria mama kinafutwa na kuweka badala yake kifungu kipya cha 37 kama ifuatavyo:

"37. Naibu Mrajis atateuliwa na Jaji Mkuu kutoka miongoni mwa Naibu Warajis wa Mahakama Kuu".

## SEHEMU YA TANO
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MADAWA NA USAMBAZAJI HARAMU WA MADAWA YA KULEVYA, NAM. 9 YA 2009

Kusomwa.

**10.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Madawa na Usambazaji Haramu wa Madawa ya Kulevya, Nam. 9 ya 2009, na katika sehemu hii itajulikana kama Sheria mama.

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**11.** Kifungu cha 4(2) cha Sheria mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta aya ya (a) na badala yake kuweka aya mpya ya (a) kama ifuatavyo:

"(a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Rais;

(b) kufuta aya ya (b);

(c) kupanga upya aya zilizobaki kwa mpangilio wake.

Marekebisho ya kifungu cha 5.

**12.** Kifungu cha 5(2) cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta maneno "wa Nchi Afisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais" baada ya neno "Waziri".

Marekebisho ya kifungu cha 63.

**13.** Kifungu cha 63(1) cha Sheria mama kinafutwa na badala yake kuweka kifungu kipya cha 63(1) kama ifuatavyo:

Uwezo wa kutunga Kanuni na Miongozo.

**63.**-(1) Kwa kuzingatia masharti mengine ya Sheria hii, Waziri anaweza, kutunga Kanuni na Miongozo kwa ajili ya utekelezaji bora wa madhumuni ya Sheria hii.

## SEHEMU YA SITA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MASHIRIKIANO BAINA YA SEKTA YA UMMA NA SEKTA BINAFSI, NAM. 8 YA 2015

Kusomwa.

**14.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mashirikiano baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi, Nam. 8 ya 2015, na katika sehemu hii itajulikana kama Sheria mama.

Marekebisho ya kifungu cha 2.

**15.** Kifungu cha 2 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta tafsiri ya neno "Waziri" na badala yake kuweka tafsiri mpya kama ifuatavyo:

"Waziri" maana yake ni Waziri anaehusika na mambo ya fedha;

(b) kuongeza tafsiri ya neno "hatua ya mwisho ya kifedha" katika mpangilio wake wa herufi kama ifuatavyo.

"hatua ya mwisho ya kifedha" maana yake ni wakati wa hatua ya mwisho ya kuwekwa saini ya makubaliano ya mradi na kifedha.

Marekebisho ya kifungu cha 21.

**16.** Kifungu cha 21 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta aya ya (c) na badala yake kuweka aya mpya ya (c) kama ifuatavyo:

"(c) kurejesha fedha zilizotumika kutokana na taratibu za mashirikiano baina ya sekta ya umma na sekta binafsi katika hatua ya mwisho ya kifedha;"

Marekebisho ya kifungu cha 35.

**17.** Kifungu cha 35(2) cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufutwa aya ya (c) na kuweka badala yake aya mpya ya (c) kama ifuatavyo:

"(c) thamani ya fedha iliyopo ndio thamani ya malipo itakayolipwa baadae na Mamlaka, kama yapo:"

Marekebisho ya kifungu cha 38.

**18.** Kifungu cha 38 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta kifungu kidogo cha (5) na kuandika upya kama ifuatavyo:

"(5) Afisi ya Mwanasheria Mkuu itatoa ushauri wa kisheria kwa Wizara ya Fedha ndani ya kipindi cha miezi miwili kuhusiana na makubaliano husika".

Marekebisho ya kifungu cha 46.

**19.** Kifungu cha 46(3) cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kufuta aya ya (f) na badala yake kuandika upya kama ifuatavyo:

"(f) masharti yoyote yanayohusiana na taasisi ya kibiashara kama taasisi ya kisheria, ikijumuisha kiwango cha chini cha mtaji wa taasisi, iliyoanzishwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria".

## SEHEMU YA SABA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA NAM. 4 YA 2015

Kusomwa.

**20.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma Nam. 4 ya 2015, na katika sehemu hii itajulikana kama Sheria mama.

Marekebisho ya Jadweli la pili.

**21.** Sheria mama inarekebishwa katika Jadweli la pili kama ifuatavyo:

(a) katika Sehemu ya Pili, kwa kufuta chati (c) na badala yake kuweka chati mpya (c) kama ifuatavyo:

**(c) Fedha katika akaunti ya Benki au taasisi ya fedha iliyopo nje ya Zanzibar (Taja nchi ambazo unamiliki akaunti ya Benki)**

| (1) Jina la Benki, Taasisi ya Fedha na mahala *ilipo* | (2) Nambari ya Akaunti | (3) Kiwango | (4) Chanzo cha Fedha | (5) Faida kutoka kwenye Akaunti | (6) Matumizi Binafsi/ Biashara |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |
| | | | | | |

(b) katika Sehemu ya tatu, kwa kufuta chati (g) na badala yake kuweka chati mpya (g) kama ifuatavyo:

**(g) Vyombo vya moto na chombo chengine cha usafiri (boti, ndege, mashine ya moto) iliyopo Zanzibar au nje ya Zanzibar.**

| (1) Aina | (2) Nambari ya Usajili | (3) Nambari ya chesesi | (4) Thamani | (5) Chanzo cha matumizi ya fedha | (6) Pahala ilipo | (7) Matumizi Binafsi/ Biashara |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |
| | | | | | | |

SEHEMU YA NANE
MAREKEBISHO YA SHERIA YA BIASHARA
NAM. 14 YA 2013

Kusomwa.

**22.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Biashara Nam. 14 ya 2013, na katika sehemu hii itajulikana kama Sheria mama.

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**23.** Kifungu cha 3 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kuongeza tafsiri ya neno "mashine ya kieletroniki ya kutolea risiti" katika mpangilio wake wa herufi kama ifuatavyo:

"mashine ya kielektoniki ya kutolea risiti" maana yake ni mashine iliyoundwa kwa ajili ya matumizi katika biashara ili kudhibiti vizuri mfumo wa mauzo katika maeneo ya biashara na kudhibiti bidhaa zilizobaki ambao unakwenda sambamba na matakwa ya mashine yenyewe ikijumuisha taarifa fupi za mauzo, takwimu za kodi za kieletroniki, mashine ya kieletroniki ya kutolea risiti na mashine ya kieletroniki ya kuwekea saini.

Marekebisho ya kifungu cha 23.

24. Kifungu cha 23 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo cha (2) mara baada ya kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

"(2) Kunaanzishwa matumizi ya mashine ya kieletroniki ya kutolea risiti kwa madhumuni ya kudhibiti mapato ya Serikali yanayotokana na miamala sahihi ya kibiashara pamoja na upatikanaji wa takwimu sahihi"

SEHEMU YA TISA
MAREKEBISHO YA SHERIA YA CHUO CHA KILIMO CHA KIZIMBANI,
NAM. 5 YA 2007

Kusomwa.

**25.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Chuo cha Kilimo cha Kizimbani, Nam. 5 ya 2007, na katika Sehemu hii itajulikana kama Sheria mama.

Marekebisho ya kifungu cha 7.

**26.** Kifungu cha 7 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (2) mara baada ya kifungu kidogo cha (1) kama ifuatavyo:

"(2) Baraza linaweza kuanzisha Kamati ya Utafiti na kamati nyenginezo kwa ajili ya utekelezaji mzuri wa kazi za Baraza"

Marekebisho ya kifungu cha 9.

**27.** Kifungu cha 9 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) kwa kuingiza neno "Mkuu" baada ya neno "Mkurugenzi" katika kifungu kidogo cha (1) na kila katika vifungu vyenginevyo vya Sheria hii.

(b) kwa kuongeza kifungu kidogo kipya cha (5) baada ya kifungu kidogo cha (4) kama ifuatavyo:

"(5) Rais anaweza kuteua Naibu Mkurugenzi Mkuu ambaye atatekeleza kazi zake kwa maelekezo ya Mkurugenzi Mkuu".

## SEHEMU YA KUMI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MFUKO WA JIMBO, NAM. 4 YA 2012

Kusomwa.

**28.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mfuko wa Jimbo, Nam. 4 ya 2012 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama Sheria Mama.

Marekebisho ya kifungu cha 9.

**29.** Kifungu cha 9 cha Sheria mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) katika kifungu kidogo cha (2) kwa kuongeza aya mpya ya (e) mara baada ya aya ya (d) kama ifuatavyo:

"(e) Mkurugenzi wa Serikali ya Mtaa husika ambaye atakuwa Katibu wa Kamati"

(b) kwa kufutwa kifungu kidogo cha (3) na kuweka badala yake kifungu kidogo kipya cha (3) kama ifuatavyo:

"(3) Kamati inaweza kumualika mtaalamu yeyote kuhudhuria vikao vya Kamati,pale itakapoona inafaa, kwa ajili ya kutoa ushauri, lakini mtaalamu huyo hatokuwa na haki ya kupiga kura"

## SEHEMU YA KUMI NA MOJA
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA ZANZIBAR, NAM. 7 YA 2014

Kusomwa.

**30.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Mamlaka za Serikali za Mitaa Zanzibar Nam.7 ya 2014 ambayo katika sehemu hii itajukana kama Sheria Mama.

Marekebisho ya kifungu cha 4.

**31.** Kifungu cha 4 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingizwa kifungu kidogo kipya cha (4) mara baada ya kifungu kidogo cha (3) kama ifuatavyo:

"(4) Mamlaka za Serikali za mitaa zitakua katika ngazi ya uongozi wa Wilaya".

Marekebisho ya kifungu cha 10.

**32.** Kifungu cha 10 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika aya ya (c) kwa kufutwa neno "Baraza la Shehia" na kuweka neno jipya "Kamati ya mashauriano ya Shehia" katika kifungu hiki na popote litakapojitokeza katika Sheria hii.

Marekebisho ya kifungu cha 11.

**33.** Kifungu cha 11 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) Katika kifungu kidogo cha (2) aya ya (a) kwa kufuta neno "Chombo kinachojiendesha kibiashara" na kuweka neno "Chombo kinachojitegemea" katika kifungu hiki na popote litakapojitokeza katika Sheria hii.

(b) Kufuta aya ya (b) na kuweka ifuatayo:

"(b) Baraza la Manispaa litakua ni Chombo kinachojitegemea, litagaiwa kwa idadi ya wadi kama itakavyoamuliwa na Waziri kwa mujibu wa sifa kama ilivyoelezwa katika Jadweli la pili.

(c) Kufuta aya ya (c) na kuweka ifutayo:

(c) Baraza la Mji litakua ni Chombo kinachojitegemea, litagaiwa kwa idadi ya wadi kama itakavyoamuliwa na Waziri kwa mujibu wa sifa zilizoelezwa katika Jadweli la pili.

(d) Kufuta kifungu kidogo cha (4) na kuweka kifungu kifuatacho:

"(4) Baraza la Halmashauri ya Wilaya litakua ni Chombo kinachojitegemea, litagaiwa kwa idadi ya wadi kama itakavyoamuliwa na Waziri na kwa mujibu wa sifa kama ilivyoelezwa katika Jadweli la pili.

Marekebisho ya kifungu cha 12.

**34.** Kifungu cha 12 cha Sheria Mama kinarekebishwa katika kifungu kidogo cha (3) kwa kufuta neno "Jadweli la tatu" na kuweka neno "Jadweli la pili".

Marekebisho ya kifungu cha 22.

**35.** Kifungu cha 22 cha Sheria Mama kinarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) katika kifungu kidogo cha (1) aya ya (a), kufuta neno "Meya" na kuweka neno jipya "Mwenyekiti".

(b) katika kifungu kidogo (1) aya ya (b), kufuta neno "Naibu Meya" na kuweka neno jipya "Makamo Mwenyekiti.

Marekebisho ya kifungu cha 26.

**36.** Kifungu cha 26 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuongeza aya mpya ya (t) kama ifuatavyo:

" (t) kukataza au kuweka utaratibu wa ufugaji wa Ng'ombe, kuku , kudhibiti uzururaji wa wanyama kiholela, kuweka Wanyama na kudhibiti Wanyama wa aina yoyote nyengine ndani ya eneo lililoainishwa katika Mamlaka za Mitaa"

Marekebisho ya kifungu cha 30.

**37.** Kifungu cha 30 cha Sheria Mama kinarekebishwa kwa kuingiza kifungu kipya kidogo cha (4) mara baada ya kifungu kidogo cha (3) kama ifuatavyo:

"(4) Wakati Baraza litakapovunjwa, Meya na Naibu Meya, Mwenyekiti na Makamo Mwenyekiti wakiwa bado wanaendelea kuwepo katika Afisi hawatakuwa na uwezo wa kufanya kazi za Baraza.

Marekebisho ya kifungu cha 88.

**38.** Kifungu cha 88 cha Sheria Mama kinafutwa na kuwekwa kifungu kipya cha 88 kama ifuatavyo:

Uwezo wa Waziri wa kulivunja na kuliitisha Baraza

88.-(1) Waziri amepewa uwezo wa kulivunja Baraza kwa ajili ya kufanyika Uchaguzi Mkuu au kulivunja kabla ya kutimia muda wake; wakati wa kuvunjwa Baraza , Uchaguzi wa Madiwani utafanyika na Baraza jipya litaitishwa na Waziri kukutana na kufanya mkutano wa mwanzo si zaidi ya siku tisini (90) kutoka tarehe ya kuvunjwa kwa Baraza.

(2) Pale ambapo thuluthi mbili ya Madiwani wamepeleka Ombi kwa Waziri pamoja na sababu za kulivunja Baraza kabla ya muda wake kumalizika, Waziri ndani ya siku kumi na nne kutoka tarehe aliyopokea Ombi hilo atafanya yafuatayo:

(a) Kufanya Uchunguzi kama sababu zilizoelezwa katika Ombi zinatosha kulivunja Baraza na kamaataridhika atalivunja Baraza;

(b) Ikiwa itaonekana sababu ya kulivunja Baraza hazitoshelezi, Waziri atalikataa ombi hilo;

(3) Waziri atakapolivunja Baraza chini ya kifungu cha 88 (2) (a) cha Sheria hii, atatoa taarifa kwa Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar kutokana na Amri hiyo.

## SEHEMU YA KUMI NA MBILI
## MAREKEBISHO YA SHERIA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI
## NAM. 4 YA MWAKA 1998

Kusomwa.

**39.** Sehemu hii itasomwa pamoja na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani namba 4 ya mwaka 1998 ambayo katika sehemu hii itajulikana kama Sheria mama.

Marekebisho ya kifungu cha 3.

**40.** Kifungu cha 3 cha Sheria mama kinarekebishwa kwa:

(a) kufuta maneno "kuanzia na baada ya tarehe 1 Januari, 1999" yaliyopo katika kifungu kidogo cha (1);

(b) kufuta kifungu kidogo cha (2) na kuweka kifungu kidogo chengine kipya cha (2) kama ifuatavyo:

"(2) Bila ya kujali masharti ya Sheria hii, Waziri ataweka utaratibu wa Kanuni ya malipo ya VAT kwa manunuzi ya bidhaa kutoka Tanzania Bara".

(c) kufuta kifungu kidogo cha (3) na (4).

**Umepitishwa** na Baraza la Wawakilishi, tarehe 24 Septemba, 2016.

**{ RAYA ISSA MSELLEM }**
**KATIBU, BARAZA LA WAWAKILISHI**
**ZANZIBAR**